HALIUZWI

SAUTI YA

# TUICO

TOLEO NA: 28

OKTOBA - DISEMBA 2024




# TUICO MBELE DAIMA

## ‘’MSHIKE MKONO MFANYAKAZI JIRANI YAKO AJIUNGE NA TUICO’’

2

# YALIYOMO:

**BODI YA UHARIRI:**

Mwenyekiti

B.Y. Nkakatisi, Katibu Mkuu

MHARIRI MKUU

Venance Majula

Afisa Habari na Mawasiliano

**WAJUMBE:**

Peles Jonathan Hageze
Innocent Alute
Willy Kibona
Wakili Noel Nchimbi
Silpha Kapinga
Margaret Ndagile
Sylvester Issaya
Lisungu Mapunda
Issa Sadallah
Beatrice Ouko
Eliada Mabagala
Exavery Ngowi
Sevio Shanes Nungu



TAARIFA MUHIMU ZA CHAMA..........................ii

UJUMBE KUTOKA KWA KATIBU MKUU....................iii

HABARI................................................ 12 - 37

UTATUZI WA MIGOGORO Pg 12

MIKATABA YA HALI BORA

KWA WAFANYAKAZI Pg 15-16

TAARIFA MKUTANO WA WAFANYAKAZI

NA WANACHAMA TUICO DAWASA Pg 17-18

WAGENI WALIO TEMBELEA

TUICO MAKAO MAKUU Pg 20-21

MIJADARA YA WANAWAKE Pg 22-23

TUICO YA TOA MAFUNZO YA

TEHAMA KWA WATENDAJI Pg 24,25,26

MUKHTASARI WA TAARIFA YA KAZI KWA

KIPINDI CHA JANUARI HADI DISEMBA 2023 Pg 27-37

UNYANYASAJI WA KIJINSIA MAHALA PAKAZI 39-41

MATUKIO KATIKA PICHA:

MAKALA:

SHAIRI:

# UTANGULIZI:

TUICO ni Chama huru cha wafanyakazi wa viwanda,Biashara, Taasisi za Fedha, Huduma na Ushauri. Licha ya mchakato wa kuunda Chama kuanza mwaka 1991, TUICO kilisajiliwa rasmi tarehe 1 Januari, 1996 na kupata namba ya usajili Na: 01. Lengo kuu la chama siyo kujipatia kipato au wala siyo kuwakumbatia wafanyakazi wazembe au wahalifu, bali kuzitetea haki na maslahi ya wanachama wake na kwamba wafanyakazi wanapewa heshma na kuthaminiwa sehemu ya kazi.



**DIRA YA CHAMA**

Kuwa Chama imara na cha kidemokrasia kinachotoa huduma bora kwa Wananachama wake.

**DHAMIRA YA CHAMA**

Kutoa huduma bora zinazokizi mahitaji ya wanachama.


**MISINGI YA CHAMA**

i. Uhuru wa wafanyakazi
ii. Umoja na Mshikamano
iii. Demokrasia na Nidhamu
iv. Uongozi na Uwajibikaji
v. Uwazi na Ukweli
vi. Utawala na Sheria
vii. Haki na Wajibu
viii. Usawa na Heshima
ix. Elimu

# UTANGULIZI:



**MWANYEKITI TUICO TAIFA**



**KATIBU MKUU**



**NAIBU KATIBU MKUU & MKUU SEKTA YA FEDHA**



**MKUU WA SEKTA YA HUDUMA NA USHAURI**



**MKUU WA SEKTA YA VIWANDA**



**MKUU WA SEKTA YA BIASHARA**

# SEKTA KUU NDANI YA CHAMA

Ili kuwa na uwajibikaji wa pamoja na kutekeleza kwa ufanisi shughuli zake,Chama kina sekta kuu nne ambazo zinaongozwa na Makatibu wa Kuu na Wasaidizi.

Sekta hizo ni sekta ya Viwanda Biashara, Huduma na Ushauri

**HUDUMA ZINAZOTOLEWA NA CHAMA**

TUICO inayo majukumu makuu yafuatayo.
i.Kutetea haki za wafanyakazi/wanachama

ii. Kufunga mikataba ya Hali Bora ya Wafanyakazi kwa lengo la kuboreshaa

iii. Kuhakikisha kuwa mahusiano mema miongoni mwa wadau yanadumu

iv. Kishirikiana na waajiri katika kudumisha uwajibikaji na mazingira mazuri mahali pa kazi.

**UHURU/HAKI YA KUJIUNGA NA CHAMA**

Kimsingi mfanyakazi yeyote anao uhuru wa kujiunga na chama kama ilivyo ainishwa chini ya kifungu cha 9 cha Sheria ya Ajira na Mahusiana Kazini ya mwaka 2004.

TUICO inamkaribisha mfanyakazi yeyote kujiunga na Chama ili aweze kunufaika na huduma zinazotolewa na Chama.



*Katibu wa TUICO mkoa akitoa semina kwa wafanyakazi kabla ya kuwasajili kujiunga na chama*





# KARIBU KUSOMA TOLEO LA 28 LA JARIDA LA SAUTI YA TUICO.

**NDUGU MSOMAJI**

TUICO ni chama huru cha Wafanyakazi wa Viwanda , Biashara, Taasisi za fedha , Huduma na Ushauri kilichosajiliwa chini ya Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Wafanyakazi Tanzania kwa Lengo la kudai, kulinda na kutetea haki, heshima na maslahi ya Wanachama wake na Wafanyakazi kwa ujumla.

Kwa zaidi ya miaka 20 sasa tumeendelea kuboresha hali ya Wanachama na Wafanyakazi katika Maisha yao na wakati wote wakiwa kazini. Tunashirikiana na kujadiliana na Waajiri katika kuunda kamati za majadiliano na kuanzishwa kwa mabaraza ya Wafanyakazi ilikudunisha amani na utulivu Mahala pakazi.

Aidha, tumeendelea kujadiliana na kuondoa tofauti zinazojitokeza baina ya Mwajiri na Mwanachama au Mwanachama mmoja na Mwingine kwa njia ya Makubaliano ya amani kila itakapo wezekana sambamba na kujadili na kufunga mikataba ya Hali Bora za kazi, Tuzo, kanunu za utumishi na sheria nyingine za kazi zitumikazo nchini.

Tunawasiliana na Serikali kuhusu utungwaji wa sheria sahihi za kazi na kuunda sera nzuri za kuendeleza Uchumi na Maisha ya jamii sambamba na kulinda maslai ya Wanachama kwa kusaidia serikali ilikuepukana na uaandaaji wa sera ambazo hazina manufaa kwa Wafanyakazi.

Katika kuongeza tija na ufanisi wa shughuli zetu ,tumeendelea kushirikiana na Vyama vingine vya Wafanyakazi ndani nan je ya nchi ilikubadilishana ujuzi na taarifa katika masuala yanayo husiana na hali wafanyakazi na taratibu za kitaifa Sambamba na kudumisha uhusiano mwema baina ya wadau muhimu wa sekta ya kazi na ajira nchini.

**Shughuli zetu**

Kwanza, tunamtetea Mwanachama dhidi ya dhuluma , uonevu, ubaguzi na migogoro mbalimbali baina ya Mwajiri na Mfanyakazi.

Pili, tunafunga mikataba ya Hali Bora za kazi sehemu za kai kwa lengo la kuboresha Maisha ya Wafanyakazi.

Tatu, tunadumisha uhusiano mwema baina ya Wafanyakazi , mwajiri ,TUICO na Serikari na hivyo kuongeza tija na ufanisi kwa faida ya wahusika wote.

Nne, tunashirikiana na mwajiri kuhakikisha makundi ya Wafanyakazi yanafanya kazi katika Mazingira mazuri safi kiafya na kiusalama

Tano, tunashirikiana na mwajiri kuhakikisha makundi Maaluma (Wanawake, vijana na watu wenye ulemavu) yanapata haki sawa na wafanyakazi wengine katika mazingira salama. Sita, tunatoa elimu kwa wafanyakazi kuhusu sheria za kazi, haki za Mfanyakazi na maswala ya afya na usalama.

Natumaini kupitia jarida hili utafahamu kuhusu maana, shughuli kuu, mafanikio na matarajio ya Chama chetu, Chama cha Wafanyakazi waViwanda, Biashara, Taasisi za Fedha Huduma na Ushauri (TUICO).

Kupitia juhudi zetu za kufanya majadiliano na waajiri na wadau wengine wa sekta ya kazi na ajira, tumefanikiwa kuimarisha mikataba ya ajira, kuongeza mishahara na marupurupu, kuboresha mazingira ya kazi, na kuwezesha upatikanaji wa elimu na mafunzo kwa Wanacha wetu. Tumeweza kushiriki katika michakato ya sera na maamuzi ambayo yanaathiri Wanachama na Wafanyakazi na kusaidia kuleta mabadiliko Chanya katika ulimwengu wa kazi.

Mtumaini yetu ni kuendeleza mafanikio haya nakuimarisha nafasi yetu kama sauti ya Wafanyakazi nchini. Tunatarajia kufanya kazi kwa karibu zaidi na Waajiri, serikali , Asasi za kiraia, Mashirika yasio ya Kiserikali, na Wadau wengine ili kujenga mazigira bora zaidi ya kazi na kuwezesha maendeleo ya Wanachama na Wafanyakazi wote nchini. Tukisimama imara na kwa mshikamano, tunaweza kufanikisha mengi zaidi.

Naamini Pamoja tunaweza kuleta mabadiliko Chanya na kuchangiza kazi na ajira za staha ,maendeleo endelevu kwa Wafanyakazi na jamii kwa ujumla.

**Mshikamano Daima!**
**B.Y.Nkakatisi,**
**Katibu Mkuu, TUICO.**




# JIUNGE NA TUICO SASA

**NA PAUL E. SANGEZE**
**MWENYEKITI TUICO - TAIFA**

Chama cha wafanyakazi wa Viwanda ,Biashara,Taasisi za Fedha, Huduma na Ushauri (TUICO). Kimejikita katika kutoa huduma kwa Wafanyakazi na Wanachama nchini Tanzania.

Katika kutekeleza Majukumu yake Chama kinafwata mpango mkakati wa Chama ambao umepangwa kitaalamu kabisa.

Mpango mkakati wa Chama ni wa miaka mitano(5) Ambapo utekelezaji wake umegawanywa kwa kipindi cha mwaka mmoja (1)

Kazi zinazo tekelezwa kwa mujibu wa mpango huu nikama zifwatazo

- Kutoa Elimu kwa Wafanyakazi, Wanachama ,Viongozi na Watendaji.

- Kujadiliana na Waajiri kwa ajiri ya kuboresha maslai ya Wafanyakazi kupitia Mikataba ya Hali Bora za kazi.

- Kutatua migogoro ya kikazi mahala pakazi

- Kufanya mikutano,ziara na vikao ilikubaini changamoto zinazo wakabili Wanachama na Wafanyakazi na kuzitafutia ufumbuzi.

- Kuunda kamati na Matawi mahala pakazi ilikurahisisha utoaji huduma kwa Wafanyakazi Katika kipindi cha mwaka 2023 chama kilifanikiwa kwa kiasi kikubwa Kutekeleza majukumu yake kama yalivyo ainisha katika mpango kazi-

- Chama kiliwahamasisha Wafanyakazi na kupata Wanachama wapya 10242

- Mabaraza 189 ya Wafanyakazi yaliundwa na kukutana

- Jumla ya mikataba 118ilifungwa ilikuboresha maslahi ya Wafanyakazi sehemu za kazi .

- Matawi mapya 116 yaliundwa , kamati za Wanawake 46 na Afya na Usalama 77 ziliundwa.

- Semina 2175 zilifanyika ambapo wanachama 55767 walipewa Elimu mbalimbali kuhusu Vyama vya wafanyaka.

- Mikutano 1837 na ziara 4887 zilifanyika kupitia mikutano na ziara kazi Watendaji wa Chama walipata fursa ya kukutana na wanachama na kubaini Changamoto mbalimbali na kuzitafutia ufumbuzi

- Katika kipindi cha 2023 migogoro ya Wafanyakazi iliyo tatuliwa ni 324 na katika hiyo migogoro 232 ilisimamiwa kikamilifu katika ngazi mbalimbali za utatuzi na wanachama walipata haki zao.

Hivyo Chama kitaendelea kutoa Huduma Bora za viwango vya juu kwa wanachama wote. Napenda kutoa Rai kwa Wafanyakazi wote katika Sekta za Viwanda , Biashara ,Taasisi za Fedha , Huduma na

# KUTETEA NA KUSIMAMIA MASHAURI YA WAFANYAKAZI



Ndg, GUERINOUS MGIMA
KATIBU MKUU RUVUMA/SONGEA



*Makatibu wa TUICO kutoka mikoa mbalimbali walioudhuria kikao*

Katiba kipindi cha mwezi Julai TUICO imetekeleza shughuli mbalimbali baadhi ya majukumu yaliyotekelezwa na tuico. Chama cha TUICO kupitia ofisi zake zote kwa mafanikio makubwa kimeweza kusimamia mashauri ya wafanyakazi mbele ya CMA na Mahakama Kuu.

Miongoni mwa shauri lenye mafunzo ambalo lilisimamiwa kwa mafanikio makubwa na TUICO- Songea ni shauri la mfanyakazi Emmanueli Qawoga dhidi ya Mkurugenzi NSSF.

Kwenye shauri hilo licha ya mwajiri kukata rufaa kupinga uamuzi wa CMA, Mahakama kuu Kitengo cha Kazi ilitoa hukumu na amri ya kumtaka mwajiri alimpe mfanyakazi jumla ya Tsh. 345,402,136/20.

**VIKAO NA MAFUNZO**

Licha ya kutekeleza majukumu makuu ya msingi yaliyoainishwa hapo juu, pia yapo mambo mengine ya kiutawala kama vile kuratibu na kuendesha vikao vikuu vya chama, kuratibu mafunzo ya aina mbalimbali.

Hivyo basi, TUICO imefanikiwa kuratibu na kufanyika vikao kuhusu ambapo Makatibu kutoa kila eneo walipata fursa ya kuchangia maoni kuhusu njia bora ya kuboresha shughuli za kuingiza wanachama.

Aidha, baadhi yao walipata fursa ya kueleza mbinu na mikakati wanayoitumia katika kufanikisha shughuli za kuwatafuta na kuwaingiza wanachama wafanyakazi na kuanzisha matawi na kusimamia uchaguzi wa viongozi wa matawi.

**MIKAKATI YA KUIMARISHA CHAMA**

Uhai wa Chama ni pamoja na kuongezeka kwa wanacahama na matawi ya chama.

Katika kufanikisha jambo hilo kila Ofisi imepewa malengo ya kila mwezi kuhusu kuongeza idadi ya wanachama na matawi yaliyoanzishwa na hali ya vikao kwenye matawi.

Kutokana na mikakati hiyo baadhi ya ofisi zimejitahidi sana kufikia malengo ya kuongeza idadi ya

# MIKATABA YA HALI BORA YA WAFANYAKAZI.

**NA WILLY KIBONA**

Mkataba wa hali bora kwa wafanyakazi ni moja ya nyenzo ambayo inasaidia sana katika kuwatia moyo wafanyakazi ili kuwajibika kikamilifu katika kutekeleza majukumu yao.

Pia ni kichocheo ambacho kinachangia katika kuwahamasisha waajiri kushiriki katika kufunga mikataba ya Hali Bora na wanyakazi wengi kujiunga na chama…….

Furaha na hamasa vilitawala kwa Wafanyakazi wa TIPER yaani Tanzania International Petroleum Reserves Limited tarehe18Julai 2024 baada ya Chama cha Wafanyakazi wa Viwanda ,Biashara, Taasisi za Fedha( TUICO ) Kufunga Mkataba wa Hali bora na Mwajiri TIPER ambao unaboresha maslahi ya wafanyakazi wa TIPER Wakiwa kazini na baada ya ajira kukoma kwa sababu mbalimbali na Matakwa ya Sheria za kazi.

Maono na ndoto za Wafanyakazi zilifikia baada ya kusubiri kwa muda wa zaidi ya miaka 15 bila kuwa na Mkataba wa Hali Bora za Kazi.

Mkuu wa Sekta ya Biashara Ndugu Willy Kibona aliongoza kamati ya majdiliano TUICO na kufanikisha kuwa na Mkataba huo.

Kusainiwa kwa Mkataba huu kujenga imani kubwa kwa Wafanyakazi ambao pia ni wanachama wa TUICO kuwa Nyenzo muhimu sana katika kuboresha maslahi ya wafanyakazi kazini.Aidha unainua morali ya lazi na kuepuka migogoro isiyo ya lazima

Mkataba huu umeboresha mambo mengi ikiwa ni pamoja na;

A. Mishahara
B. Posho mbalimbali
C. Ada ya shule kwa Watoto wa muajiriwa.



# MKUTANO WA WAFANYAKAZI NA WANACHAMA WA TUICO DAWASA

**NA ABDUL MKAMA**

Taifa ilifanya mkutano uliowahusisha Wafanyakazi na Wanachama wote wa DAWASA vituo yote 33 Dar es salaam Pwani.

Tulipata dhini rasmi toka menejiment ya DAWASA kufanyika kwa mkutano,pia ahadi yao ya kushiriki katika mkutano huo.

Mkurugenzi wa Rasilimali Watu akiambatana na meneja wa Rasilimali watu waliudhuria na kuzungumza na washiriki kwa niaa ya Afisa Mtendaji Mkuu.

Mkutano huo ulikuwa wenye Mafanikio makubwa kwa maana a maudhulio makubwa,kupata Wanachama wapya na upigaji Picha za viza kadi za Wanachama zilikuwa nyingi kwa vile tulishirikisha Wanachama na tuliingiza pia Wanachama wapya wengi kwa wakati mmoja.

Ifuatayo ni takwimu ya mkutano huo
1.Wafanyakazi walioudhuria - 843 2.Wanachama wa zamani - 588 3. Wanachama wapya - 244

Asilimia kubwa walipigwa picha za kadi ya uanachama.Mkutano ulianza saa 5:30 Asubuhi hadi saa 9:30 Alisiri. Ulifunguliwa na Mkurugenzi wa Rasilimali Watu kwa niaba ya Afisa Mtendaji mkuu na ulifungwa na Mkuu wa Sekta ya Viwanda kwa niaba ya katibu Mkuu.

NB; Watendaji wa TUICO Makao Makuu na Mikoa yote ambayo ina vituo vya DAWASA walishiriki kwenye mkutano huo.






*Katikati ni Katibu Mkuu Ndg Boniface Nkakatisi/Nabaadhi ya watendeji makao makuu wakiwa na Wageni kutoka Misri waliofika TUICO Makao Makuu.*

# WAGENI AMBAO WALITEMBELEA OFISI YA TUICO MAKAO MAKUU

Wageni mbali mbali wameweza kutembelea TUICO Makao Mkuu kwa lengo la kujifunza na kubadilshana Mawazo na uzoefu.

Moja ya Wageni waliotembelea ni; Vyama vya Wafanyakazi Nchini Misri Kutoka sekta ya Ujenzi na Nishati, Pamoja na CjA Migodi walitembelea TUICO na kufanya Mazungumzo na Uongozi wa TUICO na kukubaliana kuwa na mpango wa kutembeleana kati ya Tanzania na Misri kwa lengo la kubadilishana uzoefu.

Mpango utaanza mara baada ya kusaini Makubaliano ifikapo Agosti, 2024.

Katikati ni Katibu Mkuu Ndg Boniface Nkakatisi/Nabaadhi ya watendeji makao makuu wakiwa na Wageni kutoka misri ,TUICO Makao Makuu.

Uhai, Uimara wa TUICO unategemea sana na kuendelea kuimarisha hali ya mshikamano, uwajibikaji wa pamoja uliopo, na uwajibikaji wa kila mmoja kadiri ya majukumu na malengo aliyowekewa.

Mafaniko ya mambo hayo yanapaswa Kwenda sambamba na kanuni ya 7ks ambazo ni;. Kupendana, Kuheshimiana, Kutekeleza malengo, Kusaidiana, Kuaminiana, Kujituma, na Kushirikiana.

Mambo hayo yakitekelezwa kwa ukamilifu yatachangia sana kufanikiwa kwa Dira na Dhima ya TUICO

# WAFANYAKAZI WANAWAKE WATAKIWA KUENDELEA KUKAMATA FURSA YA ELIMU ILI KUFIKIA MALENGO YAO

**Na Rehema Lundanga,**
**DAR ES SALAAM**

Wafanyakazi wanawake nchini wametakiwa kuweka katika vipaumbele vyao suala ya kujiendeleza kielimu ili kuweza kuleta mabadiliko katika sehemu zao za kazi sambamba na kujiimarisha kiuchumi.

Wito huo umetolewa na Mbunge wa Viti Maalumu anayewakilisha Wafanyakazi Mhe. Janejelly James Ntate ( MB) leo Alhamis tarehe 7 Machi 2024 alipokuwa Mgeni Rasmi katika Kongamano kubwa la Wafanyakazi Wanawake lililoandaliwa na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania ( TUCTA).

Mhe. Ntate amesema kuwa ili kuharahisha maendeleo katika taifa na Jamii kama ambavyo kauli mbiu ya mwaka huu imehimiza ni lazima kufanya uwekezaji mkubwa kwa Wanawake ikiwemo kuwaendeleza kielimu ili waweze kuleta tija na kuwa na chachu ya mabadiliko katika Sehemu zao za kazi.

Sambamba na wito huo pia amewataka wanawake kupendana, kushirikiana katika mambo mbalimbali pia wasifungie vipawa vyao ndani naye kwa upande wake kupitia nafasi yake ataendelea kuwawakilisha vyema bungeni kwa kuzisema hoja mbalimbali za Wafanyakazi anapokuwa Bungeni.

Akimkaribisha Mgeni Rasmi Mwenyekiti wa Wanawake TUCTA, Ndg. Rehema…….amevishukuru Vyama vyote vinavyounda Shirikisho hilo la Wafanyakazi kwa kushiriki kikamilifu katika Kongamano hilo na kuwataka kutumia kongamano hilo kujadiliana na kujiwekea malengo yenye Tija ili kuleta mabadiliko katika Vyama vyao na baadae kwenye Shirikisho

Kongamano hilo limehudhuriwa na Wawakilishi kutoka katika Vyama vya Wafanyakazi vinavyounda Shirikisho hilo ikiwa ni sehemu kuelekea katika kilelele cha Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani kwa mwaka huu ambapo kilele chake kitakuwa ni kesho Machi



# MAKATIBU WASAIDIZI TUICO WAKIPEWA WAFUNZO YA TEHAMA.



*Makatibu wasaidizi tuico wakipewa wafunzo kuhusiana na matumizi ya mifumo ya Tehama*

**Na Lisungu Mapunda**

TUICO yajidhatiti katika matumizi ya mifumo ya kielectronic ili kutunza, kutuma, taarifa za ofisi kwa mfumo wa kidigitali kama vile taarifa za wanachama wapya, ada, Mikataba ya Hali Bora za Kazi, taarifa ya matukio ya ajali mahali pa kazi na namna zilivyoshughulikiwa, taarifa za mikutano, semina na kamati mbalimbali zilizoundwa mahali pa kazi.

Aidha TUICO imejenga miundo mbinu ya kielectronic ya kutunza taarifa za fedha, kuendesha, mikutano, mafunzo na semina kwa njia kidigitali. Aidha TUICO ina mitandao ya kijamii ambayo inalenga kuwahabarisha wanachama na wadau mbalimbali wa masuala ya kazi kuhusu utekelezaji wa shughuli mbali mbali za Chama pamoja na mafanikio yaliyopatikana ya Chama.

Pia matumizi ya mitandao ya kijamii inalenga kutoa fursa ya wanachama na wafanyakazi kupata taarifa kutoka kwenye vyanzo rasmi na kwa wakati muafaka. Katika kufanikisha zoezi hili Chama kimekuwa kikiendesha mafunzo ya matumizi ya mitandao ya kidigitali kwa watendaji wake.

Katika mafunzo yaliyofanyika hivi karibuni mjini Morogoro tarehe 27 Julai 2024, Chama kilifanikiwa kutoa mafunzo ya matumizi ya mtandao unaojulikana kama TUICO Management Information System (MIS) kwa baadhi ya Makatibu wasaidizi wakitoka Mikoa mbalimbali.

Lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo watendaji hao lakini pia wawe chachu ya utekelezaji wa matumizi ya mifumo ya kidigitali ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa shughuli za Chama.

Mafunzo kama haya yataendelea kutolewa mara kwa mara ili watendaji wa Kada mbalimbali waweze kujijengea uwezo na hatimaye kupunguza matumizi ya karatasi ofisini ili angalao hadi kufikia mwishoni mwa mwaka 2025 kiwango cha matumizi ya karataisi kama njia ya mawasiliano yapungue na badala yake mawasiliano kati ya ofisi za Chama za Matawi, Mikoa, Kanda na Makao Makuu yaweze kufanyika kidigitali. Ili kutimiza adhima hii, Chama kitaandaa mpango wa mafunzo ya TEHAMA kwa kipindi cha utekelezaji wa shughuli za Chama za mwaka 2025 chini ya udhamini kutoka Vyama rafiki vya Kimataifa.

Wenzetu Chama cha Wafanyakazi kutoka sekta ya viwanda (IndustriALL) kwa kushirikiana na Shirikisho la Wafanyakazi la Kimataifa kutoka sekta ya ujenzi (BWI) wenye Makao Makuu mjini Geneva Swetzerland na ofisi za Kanda ya Afrika mjini Johannesburg Afrika Kusini tutaandaa programu ya pamoja ya mafunzo ya kidigitali hapa Nchini.

Aidha Chama kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kitaendelea kuandaa programu mbalimbali ili matumizi ya tehama na mifumo ya kidigitali iweze kutumika kwenye mikutano, warsha, semina na hata makongamano mbalimbali kwa lengo la kuleta ufanisi wa mawasiliano miongoni mwetu.

# CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA VIWANDA, BIASHARA, TAASISI ZA FEDHA, HUDUMA NA USHAURI(TUICO)

## MUHTASARI WA TAARIFA YA KAZI KWA KIPINDI CHA JANUARI HADI DESEMBA, 2023

### 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii inaonesha shughuli zote zilizofanywa na Chama katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2023 kwa Sekta, Idara na Vitengo kwa mujibu wa Mpango Mkakati wa Chama.

Pamoja na changamoto zilizoikumba Dunia kutokana na vita kati ya Urusi na Ukraini, kupanda kwa bei ya mafuta, kushuka kwa thamani ya Shilingi dhidi ya Dola ya Marekani na uhaba wa fedha za kigeni, Chama kimeendelea kutumia fursa za ukuaji wa kiuchumi na mazingira mazuri ya uwekezaji yanayosimamiwa na Serikali ya Awamu ya Sita katika kufikia malengo yake.

Fursa hizo ni pamoja na ujenzi wa Mradi Mkubwa wa kufua Umeme wa "Julius Nyerere Hydro Power Plant (JNHPP)", Mradi wa Reli ya Mwendo Kasi (SGR), Miradi ya ujenzi wa barabara, Uanzishwaji wa Viwanda Vipya, kuimarika kwa Sekta ya Utalii na Ukuaji wa Sekta Isiyo Rasmi.

### 1.1 HALI YA KISIASA NCHINI

Katika kipindi cha Taarifa hii hali ya kisiasa Nchini imeendelea kuwa ya amani na tulivu, ambayo imewezesha wananchi kufanya kazi kwa bidii na kuendeleza ujenzi wa Taifa.

| Mwezi | Mfumuko wa Bei (%) |
|---|---|
| Januari | 4.9 |
| Februari | 4.8 |
| Machi | 4.7 |
| Aprili | 4.3 |
| Mei | 4.0 |
| Juni | 3.6 |
| Julai | 3.3 |
| Agosti | 3.3 |
| Septemba | 3.3 |
| Oktoba | 3.2 |
| Novemba | 3.2 |
| Desemba | 3.0 |

### 1.2 HALI YA UCHUMI NA KIPATO CHA MFANYAKAZI

Tanzania ni miongoni mwa Nchi chache Afrika ambazo Uchumi wake unakuwa kwa kasi ambapo mfumuko wa bei upo kwenye tarakimu moja (Single digit). Kwa mujibu wa taarifa ya Taasisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Mfumuko wa Bei kuanzia Januari Mpaka Desemba 2023 ni kama inavyooneshwa katika jedwali lifuatalo:-

### 1.3 UENDESHAJI WA SHUGHULI ZA CHAMA

Chama kimeendelea kutekeleza Mpango Mkakati katika maeneo Makuu yafuatayo:-

#### 1.3.1 MIKATABA YA PAMOJA

Mikataba ya Hali Bora za Kazi, Kutambuana, Upunguzwaji, Ada ya Huduma, Mabaraza ya Wafanyakazi na malipo ya mishahara imejadiliwa na kufungwa sehemu za kazi, kama inavyooneshwa katika jedwali lifuatalo:-

# HABARI:

| SEKTA / AINA YA MIKATABA | Hali Bora za Kazi | Upunguzwaji | Kutambuana | Mabaraza | Ada ya Uwakala | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Viwanda** | 44 | 22 | 11 | - | - | 77 |
| **Biashara** | 3 | 2 | 3 | 1 | 1 | 10 |
| **Taasisi za Fedha** | 1 | - | - | 1 | - | 2 |
| **Huduma na Ushauri** | 11 | 3 | 14 | 1 | - | 29 |
| **JUMLA** | 59 | 27 | 28 | 3 | **1** | 118 |
| **Asilimia(%)** | 50 | 23 | 24 | 2 | 1 | |

*Tanbihi:*
*Katika kipindi cha Taarifa hii Chama kimefunga Mkataba mmoja (1) wa Ada ya Uwakala. Hata hivyo baadhi ya Mikataba ya Hali Bora iliyofungwa imejumuisha kipengele cha Ada ya Uwakala na inatekelezwa.*

### 1.3.2 MABARAZA YA WAFANYAKAZI

Katika kipindi cha Taarifa hii Mabaraza ya Wafanyakazi 189 yaliundwa na kukutana kama inavyooneshwa katika jedwali lifuatalo:-

| SEKTA | IDADI |
|---|---|
| Viwanda | 2 |
| Biashara | 158 |
| Taasisi za Fedha | 18 |
| Huduma na Ushauri | 11 |
| **JUMLA** | **189** |

### 1.3.3 WANACHAMA, MATAWI NA KAMATI MBALI MBALI

**(i) WANACHAMA**

Linganisho la Wanachama kati ya Januari 2023 na Desemba 2023 ni kama inavyoonekana katika jedwali lifuatalo:-

| SEKTA | JANUARI 2023 | DESEMBA 2023 | ONGEZEKO | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| Viwanda | 66097 | 74,136 | 8039 | 12 |
| Biashara | 17229 | 18422 | 1183 | 6.8 |
| Taasisi za Fedha | 13276 | 13681 | 405 | 3 |
| Huduma na Ushauri | 12475 | 13,090 | 615 | 5 |
| **JUMLA** | **109077** | **119,329** | **10242** | **9.4** |

### (ii) MATAWI NA KAMATI

Katika kipindi cha taarifa hii linganisho la idadi ya Matawi na Kamati ni kama inavyooneshwa katika jedwali lifuatalo:-

| KIPINDI | MATAWI NA KAMATI | | |
|---|---|---|---|
| | MATAWI | KE | OHS |
| Januari 2023 | 1195 | 588 | 692 |
| Desemba 2023 | 1311 | 634 | 769 |
| **Ongezeko** | **116** | **46** | **77** |
| **Asilimia (%)** | **9.7** | **7.8** | **11.1** |

## (iii) WANACHAMA WAPYA

Jedwali lifuatalo linaonesha Wanachama wapya katika kila Mkoa:-

| NA | MKOA | WANACHAMA | | |
|---|---|---|---|---|
| | | ME | KE | JUMLA |
| 1 | Arusha | 1260 | 1882 | 3142 |
| 2 | Dodoma | 466 | 148 | 614 |
| 3 | Ilala | 1044 | 470 | 1514 |
| 4 | Iringa | 503 | 253 | 756 |
| 5 | Kagera | 126 | 90 | 216 |
| 6 | Kigoma | 179 | 59 | 238 |
| 7 | Kilimanjaro | 204 | 105 | 309 |
| 8 | Kinondoni | 369 | 368 | 737 |
| 9 | Lindi | 184 | 49 | 233 |
| 10 | Mara | 127 | 39 | 166 |
| 11 | Mbeya | 175 | 147 | 322 |
| 12 | Morogoro | 642 | 226 | 868 |
| 13 | Mtwara | 289 | 104 | 393 |
| 14 | Mwanza | 466 | 322 | 788 |
| 15 | Pwani | 625 | 311 | 936 |
| 16 | Rukwa | 385 | 43 | 428 |
| 17 | Ruvuma | 92 | 38 | 130 |
| 18 | Shinyanga | 191 | 102 | 293 |
| 19 | Singida | 216 | 122 | 338 |
| 20 | Tabora | 186 | 21 | 207 |
| 21 | Tanga | 173 | 59 | 232 |
| 22 | Temeke | 1090 | 377 | 1467 |
| 23 | Kigamboni | 293 | 62 | 355 |
| 24 | Mkuranga | 375 | 110 | 485 |
| | **JUMLA** | **9660** | **5507** | **15167** |

*Tanbihi:*

- *Wanachama wapya waliojiunga hadi 31 Desemba, 2023 ni 15167*
- *Wanachama waliokoma uanachama hadi 31 Desemba, 2023 ni 4915*
- *Ongezeko halisi la wanachama (Net Increase) ni 10252 sawa na asilimia 2*

### (ii) MATAWI NA KAMATI

Katika kipindi cha taarifa hii linganisho la idadi ya Matawi na Kamati ni kama inavyooneshwa katika jedwali lifuatalo:-

| KIPINDI | MATAWI NA KAMATI | | |
|---|---|---|---|
| | MATAWI | KE | OHS |
| Januari 2023 | 1195 | 588 | 692 |
| Desemba 2023 | 1311 | 634 | 769 |
| **Ongezeko** | **116** | **46** | **77** |
| **Asilimia (%)** | **9.7** | **7.8** | **11.1** |

**(iii) WANACHAMA WAPYA**

Jedwali lifuatalo linaonesha Wanachama wapya katika kila Mkoa:-

| NA | MKOA | WANACHAMA | | |
|---|---|---|---|---|
| | | ME | KE | JUMLA |
| 1 | Arusha | 1260 | 1882 | 3142 |
| 2 | Dodoma | 466 | 148 | 614 |
| 3 | Ilala | 1044 | 470 | 1514 |
| 4 | Iringa | 503 | 253 | 756 |
| 5 | Kagera | 126 | 90 | 216 |
| 6 | Kigoma | 179 | 59 | 238 |
| 7 | Kilimanjaro | 204 | 105 | 309 |
| 8 | Kinondoni | 369 | 368 | 737 |
| 9 | Lindi | 184 | 49 | 233 |
| 10 | Mara | 127 | 39 | 166 |
| 11 | Mbeya | 175 | 147 | 322 |
| 12 | Morogoro | 642 | 226 | 868 |
| 13 | Mtwara | 289 | 104 | 393 |
| 14 | Mwanza | 466 | 322 | 788 |
| 15 | Pwani | 625 | 311 | 936 |
| 16 | Rukwa | 385 | 43 | 428 |
| 17 | Ruvuma | 92 | 38 | 130 |
| 18 | Shinyanga | 191 | 102 | 293 |
| 19 | Singida | 216 | 122 | 338 |
| 20 | Tabora | 186 | 21 | 207 |
| 21 | Tanga | 173 | 59 | 232 |
| 22 | Temeke | 1090 | 377 | 1467 |
| 23 | Kigamboni | 293 | 62 | 355 |
| 24 | Mkuranga | 375 | 110 | 485 |
| | **JUMLA** | **9660** | **5507** | **15167** |

*Tanbihi:*

- *Wanachama wapya waliojiunga hadi 31 Desemba, 2023 ni 15167*
- *Wanachama waliokoma uanachama hadi 31 Desemba, 2023 ni 4915*
- *Ongezeko halisi la wanachama (Net Increase) ni 10252 sawa na asilimia 2*

### (iv) WANACHAMA WAPYA WALIOJIUNGA NA CHAMA KISEKTA JANUARI HADI DESEMBA, 2023.

Wanachama wapya waliojiunga na Chama Kisekta Januari hadi Desemba 2023 ni kama inavyooneshwa katika jedwali lifuatalo:-

| MIKOA | SEKTA | | | | | | | | | | | | JUMLA | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | VIWANDA | | | BIASHARA | | | FEDHA | | | H/ NA USHAURI | | | | | |
| | Me | Ke | Jml | Me | Ke | Jml | Me | Ke | Jml | Me | Ke | Jml | Me | Ke | Jml |
| Arusha | 1145 | 1794 | 2939 | 46 | 7 | 53 | 32 | 37 | 69 | 37 | 44 | 81 | 1260 | 1882 | 3142 |
| Dodoma | 317 | 9 | 326 | 32 | 9 | 41 | 28 | 32 | 60 | 89 | 98 | 187 | 466 | 148 | 614 |
| Ilala | 708 | 324 | 1032 | 191 | 38 | 229 | 120 | 86 | 206 | 25 | 22 | 47 | 1044 | 470 | 1514 |
| Iringa | 468 | 243 | 711 | 12 | 6 | 18 | 16 | 2 | 18 | 7 | 2 | 9 | 503 | 253 | 756 |
| Kagera | 88 | 59 | 147 | 8 | 11 | 19 | 7 | 7 | 14 | 23 | 13 | 36 | 126 | 90 | 216 |
| Kigoma | 100 | 33 | 133 | 4 | 7 | 11 | 1 | 2 | 3 | 74 | 17 | 91 | 179 | 59 | 238 |
| K`njaro | 83 | 36 | 119 | 17 | 9 | 26 | 17 | 25 | 42 | 87 | 35 | 122 | 204 | 105 | 309 |
| K`ndoni | 127 | 105 | 232 | 124 | 37 | 161 | 69 | 170 | 239 | 49 | 56 | 105 | 369 | 368 | 737 |
| Lindi | 93 | 29 | 122 | 6 | 2 | 8 | 7 | 6 | 13 | 78 | 12 | 90 | 184 | 49 | 233 |
| Mara | 43 | 0 | 43 | 19 | 4 | 23 | 25 | 10 | 35 | 40 | 25 | 65 | 127 | 39 | 166 |
| Mbeya | 37 | 5 | 42 | 29 | 7 | 36 | 54 | 51 | 105 | 55 | 84 | 139 | 175 | 147 | 322 |
| M`goro | 208 | 165 | 373 | 47 | 3 | 50 | 2 | 0 | 2 | 385 | 58 | 443 | 642 | 226 | 868 |
| Mtwara | 194 | 36 | 230 | 26 | 15 | 41 | 23 | 15 | 38 | 46 | 38 | 84 | 289 | 104 | 393 |
| Mwanza | 266 | 227 | 493 | 131 | 19 | 150 | 67 | 73 | 140 | 2 | 3 | 5 | 466 | 322 | 788 |
| Pwani | 579 | 292 | 871 | 28 | 11 | 39 | 13 | 5 | 18 | 5 | 3 | 8 | 625 | 311 | 936 |
| Rukwa | 312 | 26 | 338 | 7 | 5 | 12 | 1 | 0 | 1 | 65 | 12 | 77 | 385 | 43 | 428 |
| Ruvuma | 35 | 8 | 43 | 9 | 4 | 13 | 12 | 8 | 20 | 36 | 18 | 54 | 92 | 38 | 130 |
| S`nyanga | 115 | 54 | 169 | 13 | 4 | 17 | 34 | 21 | 55 | 29 | 23 | 52 | 191 | 102 | 293 |
| Singida | 178 | 77 | 255 | 9 | 21 | 30 | 7 | 4 | 11 | 22 | 20 | 42 | 216 | 122 | 338 |
| Tabora | 118 | 5 | 123 | 64 | 13 | 77 | 1 | 2 | 3 | 3 | 1 | 4 | 186 | 21 | 207 |
| Tanga | 110 | 16 | 126 | 5 | 8 | 13 | 44 | 31 | 75 | 14 | 4 | 18 | 173 | 59 | 232 |
| Temeke | 908 | 295 | 1203 | 100 | 19 | 119 | 52 | 60 | 112 | 30 | 3 | 33 | 1090 | 377 | 1467 |
| Kigamboni | 96 | 29 | 125 | 128 | 4 | 132 | 1 | 4 | 5 | 68 | 25 | 93 | 293 | 62 | 355 |
| Mkuranga | 350 | 93 | 443 | 8 | 6 | 14 | 12 | 7 | 19 | 5 | 4 | 9 | 375 | 110 | 485 |
| **JUMLA** | **6678** | **3960** | **10638** | **1063** | **269** | **1332** | **645** | **658** | **1303** | **1274** | **620** | **1894** | **9660** | **5507** | **15167** |

# HABARI:

**(V) IDADI YA WAFANYAKAZI NA WANACHAMA**

Idadi ya Wafanyakazi na Wanachama hadi tarehe 31 Desemba, 2023 ni kama inavyooneshwa katika jedwali lifuatalo:-

| SEKTA | WAFANYAKAZI | | | WANACHAMA | | KAMATI | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | ME | KE | JML | MATAWI | KE | |
| | 63,442 | 42,966 | 106,408 | 43,761 | 30,375 | 74,136 | 499 | 248 | |
| | 17534 | 5229 | 22763 | 14025 | 4397 | 18422 | 283 | 133 | |
| | 8,173 | 6,114 | 14,287 | 8394 | 5337 | 13731 | 328 | 146 | |
| Huduma na Ushauri | 11,916 | 5,738 | 17,654 | 8,764 | 4,326 | 13,090 | 201 | 110 | 123 |
| **JUMLA** | **101,065** | **60,047** | **161,112** | **74,944** | **44,435** | **119,379** | **1311** | **637** | **760** |

**1.3.4 MIKUTANO NA ZIARA SEHEMU ZA KAZI**
**(a) MIKUTANO ILIYOFANYIKA MIKOANI NA KITAIFA**

Lengo la Mikutano ni kuwa karibu na Wanachama, kujua kero zao na kuzitatua kwa wakati ili kudumisha uhusiano mwema na hatimaye kuongeza tija na ufanisi.

Hadi tarehe 31 Desemba, 2023 idadi ya Mikutano na waliohudhuria ni kama inavyooneshwa katika jedwali lifuatalo:-

| SEKTA | IDADI YA MIKUTANO | MAHUDHURIO | | |
|---|---|---|---|---|
| | | ME | KE | JML |
| Viwanda | 681 | 11200 | 5623 | 16823 |
| Biashara | 254 | 2503 | 916 | 3419 |
| Fedha | 483 | 1491 | 898 | 2389 |
| Huduma /Ushauri | 419 | 5115 | 2796 | 7911 |
| **JUMLA** | **1837** | **20309** | **10233** | **30542** |

# HABARI:

**(b) ZIARA ZILIZOFANYIKA SEHEMU ZA KAZI MIKOANI NA KITAIFA**

Idadi ya ziara zilizofanyika katika kipindi cha taarifa hii ni 4887 kama inavyooneshwa katika jedwali lifuatalo:-

| NA | SEKTA | IDADI |
|---|---|---|
| 1 | Viwanda | 2283 |
| 2 | Biashara | 716 |
| 3 | Taasisi za Fedha | 584 |
| 4 | Huduma na Usha | 1304 |
| | **JUMLA** | **4887** |

**1.3.5 SEMINA**

Idadi ya semina zilifanyika katika kipindi cha taarifa hii ni 2175 kama inavyooneshwa katika jedwali lifuatalo:-

| NGAZI | IDADI YA SEMINA | IDADI YA WASHIRIKI | | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| | | WANAUME | WANAWAKE | |
| Makao Makuu | 93 | 2625 | 938 | 3563 |
| Mikoa | 2082 | 32148 | 20056 | 52204 |
| **Jumla** | **2175** | **34773** | **20994** | **55767** |
| **Asilimia (%)** | | **62.4** | **37.6** | |

**1.3.6 KAMATI ZA MAJADILIANO**

Vikao vya Kamati za Majadiliano 137 vilifanyika katika kipindi cha Taarifa hii.

| NA | SEKTA | IDADI |
|---|---|---|
| 1. | Viwanda | 76 |
| 2. | Biashara | 28 |
| 3. | Taasisi za Fedha | 9 |
| 4. | Huduma na Ushauri | 24 |
| | **JUMLA** | **137** |

# UNYANYASAJI NA UKATILI WA JINSIA MAHALI PA KAZI

Na Witness Mwijage

## VISHARIA VYA UKATILI NA UNAYANYASAJI MAHALI PA KAZI

1 Uwepo wa mwenye mamlaka
2 Uwepo wa uhitaji
3 Uhitaji huo ni haki /stahiki
4 Kukosekana na ridhaa
5 Matumizi ya nguvu

## UNYANYASAJI WA KINJINSIA

Kumlazimisha mtu kujamiiana nawe kwa kumpa zawadi au kumpa kazi ni unyanyasaji wa kijinsia.

Kadhalika hakuna mtu anayeruhusiwa kushika viungo vya siri vya uzazi, au kukupiga busu bila ya ridhaa yako.

## MAANA YA UKATLI, UBAGUZI NA UNYANYASAJI WA KINJINSIA

***UKATILI*** ni hali ya kusababisha kwa makusudi mateso au kukosesha raha dhidi ya mtu mwingine.

***UNYANYASAJI*** vitendo vyote vinavyoelekezwa kwa mtu/watu/vikiundi kutokana najinsia yake.

***UBAGUZI*** kutokuwa na usawa baina ya watu /makundi mbalimbali.

## MAHALI PA KAZI PANAWEZA KUWA:

Mahali pa kazi inaweza kuwa hotelini, barabarani, sokono, nyumbani, mgahawani, sehemu ya kubadilishia mavazi, sehemu ya starehe, safarini, katika mafunzo

## UNYANYASAJI WA KINJINSIA

Kumlazimisha mtu kujamiiana nawe kwa kumpa zawadi au kumpa kazi ni unyanyasaji wa kijinsia.

Kadhalika hakuna mtu anayeruhusiwa kushika viungo vya siri vya uzazi, au kukupiga busu bila ya ridhaa yako.

## ATHARI ZA UNYANYASAJI WA KIJINSIA

1. Hupunguza uzalishaji katika eneo la kazi
2. Upatikanaji wa wataalamu wasiokidhi vigezo vya taaluma husika
3. Chanzo cha migogoro mahali pa kazi
4. Maambukizi ya Magonjwa mbalimbali mfano UKIMWI
5. Huariabu taswira ya kampuni /shirika
6. Msongo wa Mawazo

## NINI KIFANYIKE

- Jiamini na kuwa muwazi.
- Onyesha unamaanisha kupitia matendo yako.
- Onyesha unajua haki zako – Fanya jitihada za kujua sheria na haki zako za msingi katika kazi zako.
- Kama huna sifa (qualifications) jitume fanya kazi kwa bidii sana.
- Onyesha uko tayari kuacha kazi kuliko kudhalilishwa utu wako (Ila muhakikishie muhusika kuwa nae utamchafulia aache kazi kama wewe.)
- Usipende misaada au upendeleo bila sababu
- Turudi katika maadili.
- Usijilengeshe - Tabia hii inasababisha wanaume kuendekeza tabia ya dharau kwa wanawake.
- Makuzi ya watoto wa kiume - Walelewe kuthamini wanawake.

## NINI KIFANYIKE

Ili kuondoa unyanyasaji wa kijisnsia makazini na katika jamii hatuna budi kuzingatia yafuatayo;

- Kwanza elewa kuzaliwa mtoto wa kike siyo mkosi kwako wala siyo bahati mbaya bali ni fahari Kuu
- Kuwa muhanga (Victim) ni kutokana na jamii na mazingira na wala si jinsia yako

## NAMNA YA KUTOA TAARIFA ZA UNYANYASAJI NA UKATILI WA KIJINSIA MAHALI PA KAZI:

- Kutoa taarifa mara moja kwenye mamlaka husika kuhusu matukio ya unyanyasaji (Dawati la jinsia (polisi)au tume ya uamuzi na usuluhishi (CMA) au mahakama)
- Kutoa msaada muhimu kwa wahanga – kujaribu kutatua migogoro husika kwa mazungumzo
- Omba msaada kwa wajumbe wa Tawi au mfanyakazi mwenzio.
- Wasilisha malalamiko yako katika ofisi ya TUICO sehemu ya kazi (tawi)
- Kutokuwa na vikao vya kiuchunguzi ili kubaini uhalisia /mazingira ya unyanyasaji /ukatili huo

## NINI KIFANYIKE

Vyama vya wafanyakazi kuendeleza mapambano dhidi unyanyasaji wa kijinsia na kuhakikisha kwamba;

- Vinashughulikia malalamiko ya unyanyasaji wa kijinsia maeneo ya kazi.
- Vina mifumo katika ngazi zote inayoshughulikia masuala ya unyanyasaji wa kijinsia.
- Wajibu wa kueleimisha wanachama kuhusu unyanyasaji wa kijinsia.
- Kuandaa mafunzo kwa viongozi wa vyama.
- Kuingiza vipengele vya unyanyasaji wa kijnsia katika mikataba ya hali bora.
- Kufanya kazi kwa pamoja na waajiri, kuandaa mfumo bora wa kushughulikia malalamiko ya bughudha za kijinsia
- Kuwa na sera maeneo ya kazi.

## VIONGOZI WA MATAWI KUTOKA TANZANIA COMMERCIAL BANK (TCB) WAPEWA MAFUNZO YA JUU YA MAJUKUMU YA HALMASHAURI YA TAWI NA MBINU ZA UHAMASISHAJI.















# KIKAO CHA TATHMINI YA MPANGO MKAKATI KUANZIA JANUARI-JUNI 2024 KILICFANYIKA KATIKA UKUMBI WA NEW SAVOY HOTEL MOROGORO















# KIKAO CHA TATHMINI YA MPANGO MKAKATI KUANZIA JANUARI-JUNI 2024 KILICFANYIKA KATIKA UKUMBI WA NEW SAVOY HOTEL MOROGORO(1)













# MATUKIO

## KIKAO CHA TATHMINI YA MPANGO MKAKATI KUANZIA JANUARI-JUNI 2024 KILICFANYIKA KATIKA UKUMBI WA NEW SAVOY HOTEL MOROGORO(1)













# TUICO IKISAINI MKATABA WA NYONGEZA YA MSHAHARA NA BBC








# JITIHADA ZA CHAMA CHA TUICO KATIKA KULINDA NA KUPIGANIA KAZI ZENYE STAHA KWA WAFANYAKAZI VIJANA NCHINI TANZANIA



*Wafanyakazi vijana wanaofanya kazi zisizo rasmi wanahaki ya kupata haki zote za msingi kisheria, hapapaswi kubaguliwa na wanatakiwa kuheshimiwa kama wafanyakazi wengine wanaotoka katika sekta rasmi (ripoti ya ILO 2018)*

**Maelfu ya vijana katika nchi zinazoendelea bado wanakutana na changamoto kubwa ya kujishughulisha na kazi zisizo na staha, vijana wengi hususan wale wanaofanya kazi zisizo rasmi wanakutana na changamoto nyingi za kikazi kama vile kutojiunga na vyama vya wafanyakazi,**

Chama cha Wafanyakazi wa Viwanda, Biashara, Taasisi za Fedha, Huduma na Ushauri (TUICO) ni moja kati ya vyama huru vya wafanyakazi ambavyo vina dumisha na kuendelezea kazi zenye staha katika maeneo mbalimbali ya kazi.

Maelfu ya vijana katika nchi zinazoendelea bado wanakutana na changamoto kubwa ya kujishughulisha na kazi zisizo na staha, vijana wengi hususan wale wanaofanya kazi zisizo rasmi wanakutana na changamoto nyingi za kikazi kama vile kutojiunga na vyama vya wafanyakazi, kutojiunga na mifuko ya hifadhi za jamii, kutotambulika kisheria, kutothaminiwa katika maeneo yao ya kazi, kupewa mikataba ya ajira isiyokidhi matakwa ya kisheria n.k.

Mabadiliko ya teknolojia na maendeleo ya kiuchumi yameleta mabadiliko makubwa sana kwenye ulimwengu wa kazi, na hali hiyo imepelekea baadhi ya waajiri kulazimika kuwakandamiza wafanyakazi ili kujitengenezea faida zaidi.

Ripoti ya Shirika la Kazi Duniani (ILO) ya mwaka 2017 inaelezea jinsi vyama vya wafanyakazi vinavyotakiwa kubuni mbinu mpya ambazo zitawasaidia wafanyakazi kupata haki zao zote za msingi katika kipindi hiki chenye mabadiliko makubwa ya kikazi.

Sambamba na hilo, vyama vya wafanyakazi duniani kote vimekuwa mstari wa mbele kulinda,

# MATUKIO



*Katibu wa TUICO Mkoa wa Mbeya na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Magharibi, Ndugu Riziki Thomas Mashaka akiwahamasisha baadhi ya wafanyakazi wanaofanya kazi zisizo rasmi kujiunga na Chama Mkoani humo.*



*Katibu Msaidizi wa TUICO Mkoa wa Mbeya, Ndugu Hemedi Mtoni (Kulia), Na Katibu Msaidizi wa Sekta ya Fedha kutoka TUICO Makao Makuu, Ndugu Victor Komu (kushoto) wakitoa elimu juu ya Sheria za Kazi kwa wafanyakazi wanaofanya kazi zisizo rasmi Mkoani Mbeya.*

kudai na kutetea haki na maslahi ya wafanyakazi wote hususan vijana.

Chama cha Wafanyakazi wa Viwanda, Biashara, Taasisi za Fedha, Huduma na Ushauri (TUICO) kina mchango mkubwa kwa wafanyakazi vijana nchini, na maelfu ya vijana hao wananufaika na huduma bora za Chama kama vile kupata elimu juu ya sheria za kazi, kupata Mikataba ya Hali Bora ambayo inaboresha maslahi yao ya kikazi, kupata utetezi na uwakilishi kwenye vyombo mbalimbali vya kisheria kama mahakama na kupata faida nyingine mbalimbali ambazo kiujumla zinaboresha maisha yao katika nyanja zote za kimaisha kama vile kiuchumi na kijamii.

Chama cha TUICO kinatambua mabadiliko mbalimbali yanayoukumba ulimwengu wa kazi, na kutokana na hali hiyo, Chama kimeweka mikakati bora ya kupunguza na kutokomeza changamoto hizo.

Mabadiliko ya tabia ya nchi, kukua kwa teknolojia na maendeleo ya uchumi yamesababisha vijana wengi kukumbana na kazi zisizo na staha, na wengi wao wamejikuta katika changamoto nyingi za kikazi kama vile kupata ujira mdogo, kupoteza kazi, kutotambulika kisheria na baadhi yao kushindwa kujiunga na vyama vya wafanyakazi.

Moja kati ya hatua muhimu zinazofanywa na Chama ili kukomesha hali hii ni kufanya majadiliano ya pamoja na waajiri na serikali ili kufunga Mikataba ya Hali Bora na kufanya maridhiano ya pamoja ambayo yanaboresha mashlahi ya wafanyakazi hao.

Kupitia sekta zake muhimu kama Viwanda, Biashara, Taasisi za Fedha, Huduma na Ushauri, Chama cha TUICO kimewajengea misingi bora wanachama wake vijana na kuwajengea uelewa mzuri juu ya mambo mbalimbali yanayohusu shughuli za Chama.

Hata hivyo, Chama kimekuwa na mahusiano bora na serikali, waajiri na wadau wengine wa kazi, na hali hiyo imezidi kuimairisha uwepo wa wanachama wengi vijana ndani ya Chama cha TUICO.

Kazi nyingine kubwa inayofanywa na Chama cha TUICO ni kurasimisha kazi zisizo rasmi ili kulinda, kudai na kutetea haki na maslahi ya wafanyakazi wote wanaotokea katika sekta zisizo rasmi.

*Chama cha TUICO kinaunga mkono Azimio No. 204 la Shirika la Kazi Duniani (ILO) linalosema .'' Transition from the Informal to the Formal Economy Recommendation''.*

Lengo la Chama ni kuhakikisha kuwa kazi zisizo rasmi zinarasimishwa ili kuhakikisha

# MATUKIO



*Katika picha ni Makatibu wa Ofisi ya TUICO Mbeya wakiwahamasisha wafanyakazi wa kazi zisizo rasmi kujiunga na Chama.*

kuwa wafanyakazi wote wanatokea katika sekta hiyo wanapata haki na maslahi yao kama wafanyakazi wanaotokea sekta rasmi.

Chama cha TUICO kinaamini kuwa kwa kurasimisha kazi zisizo rasmi, taifa la Tanzania litakuza maendeleo ya nchi katika nyanja zote za kimaisha na kitendo hicho kitaboresha maisha ya maelfu ya vijana wanaofanya kazi hizo.

Sambamba na hilo, Chama kinatoa elimu kwa vijana na kuwajengea uwezo mzuri juu ya mambo mbalimbali ya kikazi kama vile ujuzi wa kuajirika, kujifunza kazi mbalimbali za ufundi ambazo zinawajengea uwezo binafsi, kuzielewa vizuri sheria za kazi za ndani na nje ya nchi ili kutimiza wajibu wao na kupata haki zao za msingi kisheria.

Chama cha TUICO kinaamini kuwa ili kujenga taifa lenye nguvu na mafanikio ni lazima vijana wajiunge na vyama vya wafanyakazi, na wajitoe kwa nguvu zao zote katika kufanya kazi kwa bidii ili wakuze tija na ufanisi katika maeneo yao ya kazi.

Chama cha TUICO kinaamini kuwa vijana wa kitanzania wanawajibu wa kufanya kazi kwa bidii ili kutimiza wajibu wao wa kulipigania taifa kuondokana cha changamoto kubwa kama umasikini.

Sambamba na hilo, Chama kinaendelea kupanga mikakati bora ya kuishauri serikali kuandaa sera na mikakati mizuri itayokuza ajira za vijana nchini lakini pia Chama kianedelea kutoa elimu kwa vijana ili kuwajengea uwezo binafsi wa kujiajiri na kuajirika.

Hata hivyo, Chama kinatoa wito kwa baadhi ya waajiri kuwaruhusu vijana kujiunga na Chama kwani suala hilo ni takwa la kisheria kama inayoelezwa kwenye vifungu No. 9(1)(a)(b)3(a)(b) (c) vya Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini No. 6/2004 (Sura No. 366, Marekebisho ya Mwaka 2019)

Imeandaliwa na;
Riziki Thomas Mashaka
Katibu wa TUICO Mkoa/Kanda Mbeya/Nyanda za Juu Kusini Magharibi

# MAFUNZO NA KIKAO KAZI CHA WENYEVITI NA MAKATIBU WA MATAWI YA TUICO TANESCO & MAAFISA RASIMALI WATU WA KANDA YA NYANDA ZA JUU KUSINI MAGHARIBI.




*Baadhi ya viongozi wa matawi kutoka Mkoa wa Mbeya wakiwa katika picha ya pamoja na viongozi wa TUICO na Mkurugenzi wa Rasilimali Watu wa TANESCO Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Magharibi, Bw Frank Kachenje (wapili kutoka kushoto kwa waliokaa)*

Chama cha Wafanyakazi wa Viwanda, Biashara, Taasisi za Fedha, Huduma na Ushauri (TUICO) kwa kushirikiana na Ofisi ya TANESCO Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Magharibi waliendesha mafunzo na kikao kazi cha wenyeviti na makatibu wa matawi ya TUICO TANESCO pamoja na Maafisa Rasilimali Watu wa TANESCO Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Magharibi.

Mafunzo hayo yalifanyika wilani Chunya, Mbeya kuanzia tarehe 22/07/2024 na kufikia tamati tarehe 24/07/2024.

Kupitia zoezi hilo muhimu, viongozi wa Chama cha TUICO kutoka Makao Makuu na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Magharibi walipata fursa nzuri ya kujumuika kwa pamoja na wenyeviti na makatibu wa matawi ya TUICO TANESCO na Maafisa Rasilimali Watu ambao waliuwakilisha uongozi wa shirikisho katika mafunzo hayo muhimu ambayo yalilenga kuboresha mahusiano ya pande zote mbili, kujengeana uwezo juu ya masuala mbalimbali ya kikazi.

Kupitia mafunzo hayo, washiriki wote walipata fursa nzuri ya kushiriki kwa pamoja katika mada mbalimbali zinazohusiana na kazi na ajira ambazo zililenga kukuza tija na ufanisi wa shirika pamoja na kuboresha mahusiano bora baina ya Chama cha TUICO na shirika la TANESCO, kuwajengea uwezo binafsi wenyeviti na makatibu wa matawi




*Viongozi wa Rasilimali Watu kutoka TANESCO Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Magharibi wakiwa na baadhi ya viongozi wa TUICO Kanda na TUICO Makao Makuu.*

**TUICO TANESCO.**

Mada zilizofundishwa ni kama vile Uandishwaji wa Madaraja na Mishahara, Nyaraka za Usimamizi wa Rasilimali Watu za Shirika, Mpango Mkakati wa Shirika wa Miaka 10 (CSP-2024/25-2034/350, Wajibu wa viongozi wa Matawi ya TUICO, Kanuni na Katiba ya Chama cha TUICO, Mkataba wa Kutambuana na Mkataba wa Hali Bora, Sheria Na. 8 ya Utumishi wa Umma na Kanuni zake, Umuhimu wa Vyama vya Wafanyakazi na Uimarishaji wa Chama ndani ya Taasisi, Elimu ya Masuala ya Fedha, Elimu kuhusu Kitita kipya cha Bima ya Afya na Elimu kuhusu Muifuko ya Mafao ya Jamii.

Kupitia mafunzo hayo viongozi wote walishiriki vyema na kutoa mawazo yao juu juu ya mikakati na mbinu bora za kukuza tija na ufanisi wa shirika sambamba na kudumisha mahusiano bora yaliyopo baina ya Chama na shirika.

Mkurugenzi wa Rasilimali Watu wa shirika la TANESCO kutoka Nyanda za Juu Kusini Magharibi, Bw. Frank Kachenje alisisitiza juu ya umuhimu wa mafunzo hayo na kuwashkuru viongozi wa TUICO Kanda pamoja na Makao Makuu kwa ushiriki wao mzuri, hata hivyo, Bw. Kachenje aliwashauri viongozi wote wa matawi kusoma na kuzielewa vizuri sheria za kazi zinazotumika katika maeneo yao ya kazi ili watimize wajibu wao vizuri na kujiepusha na migogoro isiyo na tija kazini.

Viongozi wengine wa Rasilimali watu kutoka TANESCO Kanda walifundisha mada mbalimbali kama vile Upandishaji wa Madaraja kazini na kutoa elimu juu ya nyaraka za usimamizi wa Rasilimali Watu za shirika.

Bw. Robert Chakudika ambaye ni Mjumbe wa Kamati ya Majadiliano TUICO TANESCO naye alisisitiza juu ya umuhimu wa mafunzo hayo kwa kusema kuwa ‘’ Kwa miaka mingi shirika na TANESCO na Chama cha wafanyakazi TUICO wamekuwa wakiendesha mafunzo na vikao kazi mbalimbali ambavyo vimechangia kukuza tija na ufanisi wa shirika, hata kuboresha mahusiano bora baina ya pande zote mbili’’, hivyo basi, Bwana Chakudika aliwasisitiza wajumbe wote kuendelea kuchapa kazi kwa bidii ili kulisaidia shirika kuendelea kutoa huduma bora kwa wananchi pamoja na kukuza maendeleo ya taifa katika nyanja mbalimbali za kimaisha kama vile kiuchumi na kijamii.

Kwa upande mwingine, viongozi wa Chama cha TUICO nao walitumia fursa hiyo kufundisha mada mbalimbali zinazolenga kuboresha mahusiano bora baina ya shirika na Chama lakini pia walieleza kwa kina juu ya faida mbalimbali ambazo wanachama wa TUICO TANESCO wanazipata kutokana na uanachama wao.

Katibu wa TUICO Mkoa wa

Iringa, Bi Gaudensia Mbone alitoa ufafanuzi mzuri juu ya Maana na umuhimu wa Mikataba ya Kutambuana na Hali Bora na kuwajengea uwezo mzuri washiriki wote juu ya miakataba hiyo, Ndugu Riziki Thomas Mashaka, Katibu wa TUICO Mkoa wa Mbeya na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Magharibi naye alifafanua kwa kina juu ya Umuhimu wa Katiba na Kanuni za Chama lakini pia alifundisha juu ya Sheria No. 8 ya Utumishi wa Umma.

Katibu Msaidizi wa Sekta ya Bishara kutoka TUICO Makao Makuu, Ndugu George Namkinga naye alipata fursa nzuri ya kutoa mada juu ya wajibu wa viongozi wa matawi na kuwakumbusha viongozi hao juu ya majukumu yao ya kila siku katika sehemu zao za kazi, sambamba na hilo, Katibu wa Mkoa wa Rukwa, Bwana Messe Chabba aliwaelezea kwa kina juu ya umuhimu wa Chama cha wafanyakazi TUICO na kuwakumbusha wafanyakazi juu ya mambo mbalimbali yaliyofanywa na Chama ili kuboresha maslahi ya wafanyakazi hao wa shirika la TANESCO.

Wajumbe wote walishiriki kikamilifu na kupata nafasi nzuri kujumuika kwa pamoja na kutoa mawazo yao juu ya mikakati bora ya kukuza na kuendeleza shughuli za shirika la TANESCO.




*Baadhi wa viongozi wa matawi kutoka Mkoa wa Iringa wakiwa katika picha ya pamoja na viongozi wa TUICO na Mkurugenzi wa Rasimali Watu wa TANESCO Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Magharibi.*



*Ndugu Fred Ndomba, Mwenyekiti wa Tawi la TUICO TANESCO Kyela akichangia jambo katika mafunzo hayo yaliyofanyika katika eneo la Omary City Hotel katika wilaya ya Chunya Mkoani Mbeya mnamo tarehe 22-24/07/2024.*

# MCHAKATO WA NIDHAMU KWA MUJIBU WA SHERIA YA UTUMISHI WA UMMA.

**Na Wakuli Noel Nchimbi,**
**mkuu wa Idara ya sheria,TUICO.**

Katika kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya watumishi wa Umma, Mamlaka za Nidhamu zinatakiwa kuzingatia Sheria ya Utumishi wa Umma Sura ya 298; Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003; Taratibu za Uendeshaji katika Utumishi wa Umma za mwaka 2003; Taratibu Bora za Nidhamu katika Utumishi wa Umma za Mwaka 2007 na Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma za mwaka 2009 na marekebisho yake ya mwaka 2011.

Mamlaka za Nidhamu Kwa mujibu wa Kifungu cha 3 cha Sheria ya Utumishi wa Umma Sura ya 298 na Kanuni zake za mwaka 2003, madaraka ya kuwachukulia hatua za nidhamu watumishi wa Umma zipo mikononi mwa mamlaka zifuatazo:-

a. Rais, Kwa mujibu wa Kanuni ya 35(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma, 2003, Rais ni Mamlaka ya Nidhamu ya Katibu Mkuu Kiongozi.

b. Katibu Mkuu Kiongozi Kwa mujibu wa Kifungu cha 4(2) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Sura 298, Katibu Mkuu Kiongozi ndiye Mkuu wa Utumishi wa Umma.

Aidha, kwa mujibu wa Kifungu cha 4(3)(d) ni Mamlaka ya Nidhamu kwa watumishi wa Umma wanaoteuliwa na Rais. Kifungu cha 4(4) kinampa katibu Mkuu Kiongozi uwezo wa kuwa Mamlaka ya Nidhamu ya juu katika Utumishi wa Umma.

Hivyo, anaweza kumchukulia hatua za kinidhamu mtumishi mwingine yeyote kwa kadri atakavyoona inafaa.

c. Waziri Mwenye Dhamana ya Serikali za Mitaa Kifungu cha 5(1)(a)(iii) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Sura ya 298, kinatamka Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa kuwa ni Mamlaka ya Nidhamu ya Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa.

d. Watendaji Wakuu (Chief Executive Officers) Kila Mtendaji Mkuu ni Mamlaka ya Nidhamu kwa watumishi walio chini yake. Mamlaka haya yameainishwa kwenye Kifungu cha 6(1)(a) na (b) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Sura ya 298.

Mamlaka za Serikali za Mitaa Kwa mujibu wa Kifungu cha 6 (6) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Sura ya 298, Mamlaka ya Serikali za Mitaa husika ndiyo itakuwa mamlaka ya nidhamu kwa watumishi walio katika mamlaka zao. Mamlaka ya Serikali za Mitaa ni Baraza la Madiwani.

e. Wakuu wa Idara na Divisheni ni Mamlaka za Nidhamu kwa watumishi walio katika Masharti ya Kawaida (Operational Service). Taratibu zao za Nidhamu ni kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya mwaka 2004.

Aina za Uendeshaji wa Makosa ya Nidhamu. Kuna aina kuu mbili za uendeshaji wa makosa ya nidhamu kutegemeana na uzito wa kosa alilolitenda mtumishi au aina ya adhabu inayotarajiwa kutolewa na Mamlaka ya Niudhamu.
Aina hizo ni:-

a. Mwenendo wa makosa mazito [Kan. 42(1)]. Mwenendo wa makosa mazito unahusu makosa makubwa ambayo adhabu zake iwapo mtumishi mtuhumiwa atapatikana na hatia, zitapelekea mtumishi aidha kufukuzwa kazi, kuteremshwa cheo, au kupunguziwa mshahara.

b. Mwenendo wa makosa mepesi (Kan. 43). Mwenendo huu unahusu makosa madogo ambayo adhabu yake haitapelekea mtumishi kufukuzwa kazi, kuteremshwa cheo au kukatwa mshahara.

Taratibu za Nidhamu
Ili haki ionekane inatendeka kabla na wakati wa kushughulikia masuala ya nidhamu, Kifungu cha 23(2)(a)(b) na (c) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Sura ya 298 lazima kizingatiwe kwa ukamilifu.

Kifungu hicho kinasema kuwa, kabla ya kumchukulia hatua za nidhamu mtumishi, lazima masharti ya kisheria yafuatayo yatimizwe:-

- Mtumishi apewe Hati ya Mashtaka;
- Mtumishi apewe fursa ya kutosha kujitetea;
- Uchunguzi ufanywe kwenye tuhuma husika kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi wa Umma, 2003

Aidha, SEHEMU YA V ya Kanuni za Utumishi wa Umma, 2003 inafafanua kwa undani taratibu za kuzingatia katika kuendesha mashauri ya

nidhamu uwe ni kwa makosa Mazito au Mepesi.

Hatua hizo ni kama ifuatavyo:-

a. Kufanya Uchunguzi wa Awali (Kan. 36) Kabla ya kumchukulia mtumishi hatua yoyote ya kinidhamu ni vyema mamlaka ya nidhamu ikafanya uchunguzi wa awali. Hatua hii itamsaidia mamlaka ya nidhamu kugundua ukweli kuhusu tuhuma na kumwezesha kujiridhisha katika hatua ya awali kuwa mtumishi amehusika na tuhuma husika na kuwa kuna uwezekano wa kuthibitisha tuhuma dhidi yake iwapo hatajitetea ipasavyo.

b. Kutoendelea na majukumu kwa kumpumzisha (Kan. 37) Mtumishi anaweza kupumzishwa bila kusimamishwa kazi na bila kuathiri maslahi yake. Lengo ni kuzuia kosa lisiendelee kutendeka wakati uchunguzi wa awali ukifanyika.

Mtumishi hatapumzishwa kwa zaidi ya siku tisini (90).

Kama kuna haja ya kuongeza siku, Mamlaka ya Nidhamu inapaswa kuomba kwa Katibu Mkuu, UTUMISHI. Muda utakaoongezwa hauwezi kuzidi miezi miwili. Kumpumzisha kazi mtumishi kutakoma mara tu taratibu za nidhamu zikianza.

c. Kusimamishwa kazi mtumishi (Kan. 38) Mtumishi husimamishwa kazi baada ya kupewa Hati ya Mashtaka. Hatua hii ni baada ya mamlaka ya nidhamu kuridhika kuwa kuna tuhuma za kujibu dhidi ya mtumishi mtuhumiwa.

Mtumishi aliyesimamishwa kazi atalipwa si chini ya nusu mshahara wake na hataruhusiwa kutoka nje ya kituo chake cha kazi bila idhini ya mamlaka yake ya nidhamu.

d. Hati ya Mashtaka [Kan. 44(3)] Hati ya Mashtaka itaandaliwa na kusainiwa na Mamlaka ya Nidhamu. Hati ya Mashtaka itaonesha kwa ufasaha kosa na kifungu cha sheria au kanuni kinachodaiwa kukiukwa na mtumishi mtuhumiwa.

Aidha, lazima iainishe kwa ufasaha maelelzo ya shitaka ili kumwezesha mtumishi mtuhumiwa kujua tuhuma zinazomkabili ili aweze kujitetea ipasavyo.

e. Hati ya Mashtaka itaambatana na Notisi ya kumtaka mtumishi mtuhumiwa kuwasilisha utetezi wake kwa maandishi (Kan. 44(5). Mwongozo wa Tume inaelekeza watumishi watuhumiwa kupewa muda wa siku 14 kuanzia tarehe ya kupokea Hati ya Mashitaka na Notisi kuwasilisha utetezi wao.

f. Mapokezi ya Hati ya Mashtaka [Kan. 44(4)] Mamlaka ya Nidhamu lazima ihakikishe kuwa mtumishi mtuhumiwa amepokea Hati ya Mashtaka.

Pale ambapo haijulikani aliko mtumishi mtuhumiwa, Kanuni ya 57(2) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003 itumike kumpelekea Hati ya Mashtaka kwa kuiacha mahali ambapo mtumishi husika alikuwa akiishi kabla ya kutoweka au kuituma kupitia anuani yake ya mwisho.

g. Kamati ya Uchunguzi [Kan. 45(1)] Endapo mtumishi mtuhumiwa hatakiri tuhuma dhidi yake wakati akijibu Hati ya Mashtaka au iwapo ataamua kukaa kimya, Mamlaka ya Nidhamu itawajibika kuunda Kamati ya Uchunguzi.

Hata hivyo, pale ambapo utetezi wa mtumishi mtuhumiwa utaonyesha kukiri makosa wazi wazi (complete admission), Mamlaka ya Nidhamu haitaunda kamati ya uchunguzi, badala yake, itaendelea kutoa adhabu kana kwamba mtuhumiwa amepatikana na hatia baada ya Kamati ya Uchunguzi [Kan. 45(3)].

h. Sifa za Kamati ya Uchunguzi (Kan. 46) Wajumbe wa Kamati ya Uchunguzi watakuwa na sifa zifuatavyo:-

- Wawe na cheo cha Uandamizi na zaidi;
- Wawe watumishi wa Umma;
- Wawe na cheo kikubwa kuliko mtuhumiwa;
- Kamati iwe na wajumbe si chini ya wawili na si zaidi ya wanne;
- Uteuzi uzingatie jinsia.

(a) Haki za Mtumishi Anayechunguzwa (Kan. 47)

- Haki ya kujulishwa kwa maandishi kuhusu tarehe, siku muda na mahali uchunguzi utakapofanyika;
- Haki ya kuhoji mwajiri na mashahidi wake;
- Haki ya kupewa na kuhakiki vielelezo vilivyotolewa kama ushahidi dhidi yake;
- Haki ya kuleta mashahidi wake na kuwasilisha vielelezo;
- Haki ya kuwakilishwa na mtumishi wa Umma, wakili au mwakilishi wa chama chake cha wafanyakazi.
- Mtumishi mtuhumiwa au mwakilishi wake anapaswa kuwepo muda wote wa uchunguzi.

(b) Iwapo wakati wa uchunguzi kutajitokeza ushahidi mpya unaohitaji kuwepo kwa tuhuma mpya, Kamati ya Uchunguzi itatakiwa kuijulisha Mamlaka ya Nidhamu ili iandae Hati ya

Mashtaka kwa tuhuma hizo.

Mtumishi mtuhumiwa apewe fursa ya kujitetea dhidi ya tuhuma hizo mpya ndipo Kamati ya Uchunguzi iendelee kuzichunguza [Kan. 47(8); (9) na (10)].

(c) Muda wa Kuunda Kamati na Kumaliza Uchunguzi; Baada ya mtumishi mtuhumiwa kupewa hati ya mashtaka, Mamlaka ya Nidhamu inatakiwa iwe imeunda Kamati ya Uchunguzi ndani ya muda usiozidi siku 60 (Kan. 47(10).

Aidha, Kamati ya Uchunguzi inatakiwa kukamilisha uchunguzi wake katika muda wa siku sitini (60) tokea ilipoanza kufanya uchunguzi (Kan. 47(11).

Endapo Kamati itashindwa kukamilisha uchunguzi katika muda wa siku 60, itaomba Mamlaka ya Nidhamu iwaongezee muda usiozidi siku 30. Iwapo muda unaohitajika kuongezwa ni zaidi ya 30 itabidi kipatikane kibali cha Katibu Mkuu (UTUMISHI) [Kan. 47(11) na (12)].

(d) Kuhitimishwa kwa Uchunguzi (Kan. 48).

Baada ya kumaliza uchunguzi, Kamati ya Uchunguzi itawasilisha mwenendo wa uchunguzi (proceedings) na Ripoti ya Uchunguzi kwa Mamlaka ya Nidhamu. Ripoti ya Kamati ya Uchunguzi inatakiwa kukidhi vigezo vifuatavyo:-

• Itamke kama, kwa maoni ya Kamati ya Uchunguzi, tuhuma dhidi ya mtumishi mtuhumiwa zimethibitishwa au la na kutoa sababu za maoni hayo.

• Hitimisho la ripoti lazima ibainishe kwa ufasaha mazingira yote yanayosababisha Kamati kuhitimisha kuwa mtuhumiwa ana hatia au hana hatia (Aya 18.2 ya Taratibu Bora, 2007)

• Itamke jambo ambalo, kwa maoni ya Kamati, inaongezea/kupunguza uzito wa tuhuma dhidi ya mtumishi mtuhumiwa (k.m rekodi ya nyuma, kujirudia rudia kwa makosa, hali ya muhusika mwenyewe, urefu wa utumishi wake, asili ya kazi yake, afya n.k [Aya 16.10(a)-(d) ya GN.53 ya 2007]

• Itamke jambo lolote ambalo, kwa maoni ya Kamati, ni muhimu (relevant).

• Isipendekeze aina ya adhabu inayostahili kuchukuliwa dhidi ya mtumishi mtuhumiwa.

(e) Utoaji wa Adhabu (Kan. 48) Mara baada ya kupokea Ripoti ya Kamati ya Uchunguzi, Mamlaka ya Nidhamu, baada ya kutafakari ushahidi na ripoti hiyo, inapaswa kutoa uamuzi na kumjulisha mtumishi mtuhumiwa kuhusu uamuzi huo katika muda wa siku thelathini (30) kuanzia tarehe ya kupokea taarifa ya Kamati ya Uchunguzi [Kan. 48(6)].

Kushindwa kutoa uamuzi ndani ya siku 30 kutatafsiriwa kuwa mtumishi mtuhumiwa hana hatia kama inavyoainishwa chini ya Kanuni ya 48(9) inavyosema;

*"Failure to comply with requirements of sub-regulation (6) of this Regulation shall be considered that the accused public servant is not guilty of the offence".*

Katika maamuzi yake, Mamlaka ya Nidhamu inawajibika kutoa sababu za maamuzi hayo na kumjulisha mtumishi haki, muda na mamlaka yake ya Rufaa.

**MASUALA YA NIDHAMU NA MAKOSA YA JINAI (Kan. 50).**

Mtumishi anapokabiliwa na kesi ya jinai mambo yafuatayo yatazingatiwa:-

• Mtumishi hatafunguliwa mashtaka ya nidhamu mpaka kesi ya jinai iishe mahakamani.

• Mashtaka ya nidhamu yakifunguliwa kisha mashtaka ya jinai yakafunguliwa, mashtaka ya nidhamu yatasimama "stayed" mpaka mahakama itoe uamuzi.

• Akiachiwa Mahakamani kwa sababu za kiufundi (on legal technicalities), kuachiwa huko hakutakuwa kizuizi dhidi ya kufunguliwa upya mashtaka ya nidhamu na kuadhibiwa kana kwamba hakukuwa na shauri la jinai mahakamani.

**RUFAA KATIKA UTUMISHI WA UMMA**

Kwa mujibu wa Kifungu cha 25 cha Sheria, pamoja na Kanuni ya 60 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003, huanisha Mamlaka za Rufaa katika Utumishi wa Umma kama ifuatavyo:-

• Watumishi wa Umma ambao Mamlaka yao ya Nidhamu ni Katibu Mkuu Kiongozi watakata rufaa kwa Rais.

• Watumishi wa Umma ambao Mamlaka yao ya Nidhamu ni Waziri mwenye dhamana na Utumishi wa Serikali za Mitaa, Watendaji Wakuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa watakata rufaa Tume ya Utumishi wa Umma.

• Mtumishi au Mamlaka ya Nidhamu ambayo haitaridhika na Uamuzi wa Tume ya Utumishi wa Umma itakuwa na haki ya kukata rufaa kwa Rais ambaye uamuzi wake utakuwa wa mwisho.

# MAKALA:

# MABADILIKO YA TABIANCHI

**Na Lisungu Mapunda**

Mabadiliko ya tabianchi ni mabadiliko katika hali ya hewa ya dunia, yanaweza kujumuisha ongezeko la joto la dunia (global warming), mabadiliko ya mifumo ya mvua, na kuongezeka kwa matukio ya hali mbaya ya hewa kama vile vimbunga, ukame, na mafuriko.

Sababu kuu za mabadiliko ya tabianchi ni pamoja na shughuli za binadamu, hususan uchomaji wa mafuta ya kisukuku kama vile makaa ya mawe, mafuta ya petroli, na gesi asilia, ambayo hutoa gesi chafuzi kama vile dioksidi kaboni (CO2) na methane (CH4) katika anga.

Haya mabadiliko yana athari kubwa kwenye mazingira na maisha ya viumbe hai, ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa joto la dunia ikisababisha kuongezeka kwa joto la bahari na kuyeyuka kwa barafu na theluji.

Baadhi ya maeneo yanaweza kupata mvua nyingi zaidi huku mengine yakikumbwa na ukame mkali, kuongezeka kwa vimbunga, dhoruba, mafuriko, na mawimbi ya joto kuongezeka kwa viwango vya bahari, hii ni kutokana na kuyeyuka kwa barafu na upanuzi wa maji ya bahari yanapopata joto, na inaweza kusababisha mafuriko ya pwani na kupotea kwa maeneo ya ardhi.

Mabadiliko haya yanaweza kuathiri makazi ya wanyama na mimea, na baadhi ya spishi zinaweza kutoweka ikiwa haziwezi kuhamia au kuzoea mazingira mapya.

Kupambana na mabadiliko ya tabianchi kunahitaji juhudi za pamoja za kimataifa, ikiwa ni pamoja na kupunguza utoaji wa gesi chafuzi, kuhifadhi misitu, na kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala kama vile nishati ya jua na upepo. Mabadiliko ya tabianchi yanaweza kuathiri shughuli nyingi za binadamu katika nyanja mbalimbali, ikiwemo kilimo na usalama wa chakula, afya ya binadamu,rasilimali za maji, sekta ya uvuvi, sekta ya utalii, miundombinu na makazi, biashara na uchumi:

Kwa ujumla, mabadiliko ya tabianchi yana athari pana na za mbali, zinazogusa karibu kila nyanja ya maisha ya binadamu na mazingira.

**Mabadiliko ya tabianchi na athari zake kwa wafanyakazi**

Katika kudhibiti mabadiliko ya tabianchi kunaweza kuathiri idadi kubwa ya ajira za wafanyakazi kwa upande mmoja.

Kwa upande mwingine ajira mpya zitazaliwa Dunia inapitia wakati wa kuazimia kufanya mabadiliko ya kufunga mitambo inayoendeshwa kwa kutumia mafuta(diesel) hivyo kutoa moshi mkubwa ambao unakwenda kutengeneza blanketi kwenye hozon layer hivyo kusababisha joto kali ambalo linaleta athari kubwa.

Viwanda na mitambo kama hiyo ndiyo kwa asilimia kubwa bado inatumika hapa nchini na ndio maeneo ya kazi ambayo yameajiri sehemu kubwa ya wafanyakazi .

Hivyo kuzimwa kwa mitambo hii kutasababisha upotevu wa ajira kwa wafanyakazi.

Lakini pendezo mbadala la matumizi ya mitambo inayotumia mafuta ni pamoja na matumizi ya mitambo nishati ya jua au nishati (umeme).

Endapo tukifaulu kufikia hatua hii ya matumizi ya nishati mbadala maana yake ni kwamba nchi itakuwa imetengeneza ajira mpya kwa wale wenye ujuzi wa kuendesha mitambo hiyo.

Hivyo wakati Dunia inapokabiliana na mabadiliko ya tabianchi na hatua za kudhibiti hali hiyo hatuna budi kujiandaa kwani wafanyakazi ni sehemu ya Dunia.

**Vyama vya Wafanyakazi vina wajibu gani katika kipindi hiki cha mpito? (Just transition)?**

Vyama vya wafanyakazi vinawajibu wa kuendelea kutoa elimu kwa wafanyakazi juu ya mabadiliko ya tabianchi na athari zake ili waweze kuchukua hatua za kukabiliana na matokeo yake.

Hatua pendekezi ni pamoja na kuendeleza kujiendeleza katika kukuza ujuzi kwenye maeneo ya matumizi ya mitambo ya nishati ya jua na umeme.

Eneo hili kwa asilimia kubwa ni jipya na teknologia ya mitambo hii inahitaji ujuzi na ualedi wa kipekee ndio maana Vyama vya wafanyakazi vinatoa rai kwa vijana ili wajikite katika kukuza ujuzi kwenye maeneo mbadala.

Aidha kwa upande wa wanafunzi wanaojiunga na vyuoni nao pia wanawajibu wa kutoa vipau mbele kwenye kuchagua fani mbadala ili kuweza kukabiliana na upatikanaji wa ajira kwenye maeneo mbadala ya sehemu za kazi.

## SHAIRI:

# NI MWAKA WA UCHAGUZI.

1. Mitano imeshapita, uchaguzi kuwadia,
Nasema pasi utata, tuanze kusimamia,
Yasije yakatukuta, Chama chetu haribia,
Ni mwaka wa uchaguzi, tuanze sasa jipanga.

2. Kuanzia Januari, mwakani naelezea,
Hatutaki machakari, wale bora tegemea,
Ni matawi januari, uchaguzi kuanzia,
Ni mwaka wa uchaguzi, tuanze sasa jipanga.

3. Kizuri huandaliwa, hili wote twalijua,
Huanza kupangiliwa, toka chini juu pia,
Tusije tukapaliwa, fumanizi kuingia,
Ni mwaka wa uchaguzi, tuanze sasa jipanga.

4. Mikoa tutafikia, viongozi jipatia,
Si vema kung'ang'ania, wasotija kuchagua,
Umakini ongezea, walobora jipatia,
Ni mwaka wa uchaguzi, tuanze sasa jipanga.

5. Wa kanda ukifikia, umakini ongezea,
Zisije kutuumbua, uchaguzi kukosea,
Tutayavuna mabua, manyani tukichekea,
Ni mwaka wa uchaguzi, tuanze sasa jipanga.

6. Taifa tukiingia, safu yote angalia,
Ni mengi twajivunia, wameyaweka sawia,
Ni nani aso wajua, tunao twajivunia,
Ni mwaka wa uchaguzi, tuanze sasa jipanga.

7. Utulivu twahitaji, chama chetu kujengea,
Wale bora hawachuji, twawaona bado wang'aa,
Tuwaongezee chaji, hatamu kukamatia,
Ni mwaka wa uchaguzi, tuanze sasa jipanga.

8. Uchaguzi ukiisha, ni vema tathiminia,
Mazuri tutaboresha, matawini kuanzia,
Hakuna wa kupotosha, ushindi kushangilia,
Ni mwaka wa uchaguzi, tuanze sasa jipanga.

9. Wahenga walishasema, nani mie kupingia,
Ni chanda kilicho chema, kuvikwa pete sawia,
Na chama kina heshima, ulimwengu shuhudia,
Ni mwaka wa uchaguzi, tuanze sasa jipanga

10. Tukilinde chama chetu, wabaya kutoingia,
Wakazileta na kutu, Chama chetu angamia,
Sawaka hata na chatu, nafasi kutopatia,
Ni mwaka wa uchaguzi, tuanze sasa jipanga.

11. Kidogo nimegusia, yalo mema kufanyia,
Hamasa nawahusia, Chama chetu kujengea,
Tusije kuwasusia, Chama chetu tabomoa,
Ni mwaka wa uchaguzi tuanze sasa jipanga.

12. Nafasi nimeishiwa, hapa mimi naishia,
Kazini ninatakiwa, Chama chetu kujengea,
Na wewe unatakiwa, pamoja lengo fikia,
Ni mwaka wa uchaguzi, tuanze sasa jipanga.

13. Tujenge Chama imara, wadau waje ingia,
Tujenge bila papara, ahadi itatimia,
Tunao wenye busara, maelfu kwa mamia,,
Ni mwaka wa uchaguzi, tuanze sasa jipanga.

14. Tamati namalizia, ujumbe kuwatolea,
Nadhani umefikia, walengwa wote sawia,
Hakuna alosalia, ujumbe kutofikia,
Ni mwaka wa uchaguzi, tuanze sasa jipanga.

15. Hakika havijazidi, kwa kuwa ninaelewa,
Huwa mno vikizidi, washairi mwaelewa,
Kwa Chama tujitahidi, tusije tukachelewa,
Ni mwaka wa uchaguzi, tuanze sasa jipanga



Hassan Athumani Mtyota.
(VIKIZIDI NI MNO)
TUICO MAKAO MAKUU
Dar es salaam.

# Follow Us on Social Media



Let's Get Connected for Our Latest News & Updates

on X (fka Twitter) @tuicounion

on Instagram @tuicounion

on LinkedIn @tuicounion

on Facebook @tuicounion




Ilala Sharif Shamba | S.L.P 5680, Dar es Salaam
Simu +255 22 2866910, 2866959/60 | Faksi: +255 22 2866911
Baruapepe: info@tuico.or.tz | Tovuti: www.tuico.or.tz

@tuicounion | @tuicounion | @tuicounion | @tuicounion

*Jenga Chama Imara, Imarisha mshikamano.*